

## **Isimu-Ushairi: Muundo wa Majigambo\***

NGO SEMZARA KABUTA

*University of Gent, Belgium*

### UTANGULIZI

Makala hii ni sehemu ya uchunguzi niliouanzisha miaka kadhaa iliyopita huko Chuo Kikuu cha Brussels kuhusu isimu ushairi, hasa tanzu maalum za fasihi simulizi, ambazo hupatikana Afrika tu. Nazo ni majigambo na tenzi. Nitajaribu kuchambua baadhi ya nduni za kiisimu za majigambo au vivugo. Mifano mingi imechukuliwa katika lugha ya Kihaya, ambayo huitwa J22 katika uainisho wa Guthrie, na ni lugha ya huko Bukoba, magharibi mwa Tanzania, karibu na Ziwa Victoria. Nduni zitakazojitokeza zitaonyeshwa katika lugha nyingine za Kibantu, k.m. Kiyaka (H31), Kimongo (C61), Ciluba (L31), Kiluba (L33), Kinyarwanda (J61), Kinyankore (J13), Kishona (S10), Kizulu (S42), n.k. na hata katika lugha zisizo za Kibantu k.v. Kiigbo (Kwa) au Kifula (Atlantiki).

Kama walivyoonyesha Balisidya 1987, Mulokozi 1989 na wengine, tanzu za fasihi simulizi ni nyingi sana. Kwa mfano, tunaweza kutambua mazungumzo, masimulizi, maigizo, semi, ngomezi, ushairi, k.v. nyimbo na maghani. Katika makala hii, nitazidi kuzungumzia maghani, ambayo ni ushairi unaotolewa kwa kalima badala ya kuimbwa. Zipo aina mbili za maghani: maghani ya kawaida na maghani ya masimulizi. Nitajishughulisha na fani moja tu ya maghani ya kawaida, yaani sifo, hasa hizo ziiwazo majigambo, nyingine zikiwa ni tondozi, ghani-masimulizi, rara, ngano na tendi. Nduni maalumu ya majigambo ambayo huyatofautisha kabisa na tanzu nyingine ni kuwa mada yake ni mshairi mwenyewe (na kwa hiyo hutumia nafsi ya kwanza tu), maudhui ni ushujaa, virudio ni majina halisi ya kishairi. Hebu kwanza tuchunguze kidogo maana za majigambo.

Dhana ya kujisifu huwakilishwa kwa vitenzi vingi sana tofauti. Aidha, karibu vitenzi vyote ni vitenzi jirejee, yaani vina kiwakilishi jirejee *-ji-* :

- (1) kujigamba (kujifanya unajua sana); kujinaki (kujitangazia sifa, kujitakasa kuwa huna makosa); kujinata (kujiona bora kuliko watu wengine); kujitwaza (kujinata); kujiketua (kujifanya kuwa na mambo usiyokuwa nayo); kujivuna (kuhisi kuwa u zaidi kuliko wengine, kuringa); kuringa (kujiona bora kuliko watu wengine; kuwa na kiburi; kujiona); kudesa (kujionyesha kwa watu kwa kitu ulichonacho; kutia mikogo, kuringa); kujifutua; kujifaragua; kujibodoa; kujikita; kujisifu; kujitapa; kujiona; kujisikia; kujitutumua; kujitukuza; kujikweza; kujinadi; kujipambanua.

Bila shaka maneno yote haya sio sinonimi, na si shabaha ya makala hii kuchunguza tofauti za maana. Nitalijadilia neno moja tu, nalo ni 'kujigamba'. Kwanza, itiliwe

maanani kwamba fasili iliyotolewa katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (1981), yaani "jigamba *ji-fanya unajua sana; jifutua; jisifu; jifaragua*", siyo inayojitokeza katika uchambuzi wa mashairi yaitwayo 'majigambo'. Mintarafu fasili ya KKS, kujigamba huonekana kama tabia mbaya ya kuwaudhi watu wengine na kwa hiyo hustahili kulaumiwa. Majigambo ni kinyume cha majisifu au majivuno. Nayo ni sanaa muhimu katika fasihi simulizi ya Kiafrika ambayo pamoja na kutungwa kwa ufundi mkubwa, humsaidia mtu binafsi au kundi la watu kujipa moyo na kujipatia nguvu. Sanaa hii ni ya zamani sana katika Afrika, kama inavyodhihirika katika mfano wa 2 hapo chini, ambao umetokana na maandishi ya Misri ya Kale (Lichtheim 1975: 89):

(2) I was a worthy citizen who acted with his arm. I was a great pillar in the Theban nome, a man standing in the Southland. I nourished Imyotru in years of misery. Though four hundred men were in straits through it, I did not seize a man's daughter, nor did I seize his field...

Mjigambi halisi si mtu wa kawaida 'anayejifanya anajua sana', bali ni mwanasanaa ambaye bila shaka, kwanza ni mshairi na pili anajua kwa undani jambo analoliongelea.

Nomino nyambuliwa na hata nyingine ambazo hazishahibiani na kitenzi chochote, aghalabu ziko katika ngeli ya 6, kama ilivyo katika lugha nyingine za Kibantu:

(3) majigambo	majisifu
majivuno	maringo
mapambano	mashindano
mapatilizano (ugomvi wa maneno)	madaha (maringo)
magigimo (hali ya kujidai nguvu na kujikita)	makuu
matuko	

Nomino moja tu, ambayo ni neno kopwa, iko katika ngeli ya 7, nayo ni *kivugo*<sup>1</sup>. Kwa mujibu wa muundo wa neno hilo katika Kihaya, ingekuwa afadhali kuunda neno kama *kievugo*, kwa kuwa maana ya hiyo *-e-* ni kiwakilishi jirejee (*-ji-* kwa Kiswahili), ambacho ni mofimu muhimu katika tanzu inayohusika. Ijapokuwa kwa kawaida maneno mengine hutumiwa kwa wingi tu, nitatumia *majigambo* kwa wingi na *jigambo* kwa umoja.<sup>2</sup>

Kujadili taaluma ya ushairi kunasababisha utumizi wa maneno ya kipekee na hata uundaji wa istilahi maalumu. Kwa hiyo, baadhi ya maneno yamependekezwa katika makala hii kufasiria dhana maalumu zinazojitokeza katika utafiti. Nayo ni

<sup>1</sup> Kufuatana na M. Mtesigwa, wa BAKITA, neno hilo limekopwa toka lugha mojawapo ya Tanzania. Nami nafikiri lugha hiyo kuwa ni Kihaya, maana katika kazi zote za fasihi simulizi nilizozichambua huko TUKI (Julai 1994), neno linalofanana na hilo hupatikana katika Kihaya tu, likiwa *ekyebugo* (eki-e-bugo), ambalo hutamkwa [ekje uGo].

<sup>2</sup> Taz. vilevile Rubanza 1994.

kama Mkabilisho, Kijivugo, Mtanuko, n.k., ambayo yamefasiliwa hapo chini. Katika Nyongeza, yameorodheshwa maneno ya kifasihi na kiisimu yaliyotumiwa katika utafiti huu na ambayo yumkini yangemletea msomaji utata, kwa kuwa hayapatikani katika kamusi zote.

Msingi wa makala hii ni majigambo ya Kihaya. Hii ni kwa sababu katika juhudi za kukusanya majigambo katika maandishi huko Tanzania, mengi kabisa yamepatikana katika lugha ya Kihaya. Kwa hiyo, Kihaya tu ndicho kilichotumiwa kuelezea aina za majigambo. Lakini katika uchambuzi wa muundo wa majigambo, lugha nyingine zimetajwa kwa madhumuni ya kuthibitisha miundo iliyojitokeza katika Kihaya.<sup>3</sup>

Kabla ya kuzingatia jambo la muundo wa majigambo, napenda kudondoa maneno machache ya Mulokozi (1989), ambayo hugusia vizuri jambo linalohusika:

Kivugo ni ghani ya kujisifia. Kwa kawaida hutungwa na kughanwa na mhusika mwenyewe. Kivugo hutungwa kwa ufundi mkubwa, kwa kutumia mbinu kama sitiari, vidokezi, ishara, takriri, na wakati mwingine hata vina. Mjigambaji ambaye kwa kawaida ni mwanamume hujitungia shairi lake kufuatia au kufungamana na tukio maalumu katika maisha yake, kwa mfano kuingia jandoni, kuoa, kurejea kutoka vitani, kushinda jambo gumu, k.m. mnyama mkali, mchezo, kesi mahakamani, masomo, n.k.

Baadhi ya majigambo huwa ni marefu sana na yenye masimulizi ndani yake, lakini mengi ni mafupi. Vivugo vingi hueleweka kwa urahisi kwa hadhira iliyokusudiwa, kwa vile huzungumzia mambo wanayoyafahamu au waliyoyashuhudia. Wale wasiohusika hupata taabu kuvielewa, hasa kama hawaifahamu vizuri historia ya mtunzi.

Muundo wa kivugo hutegemea shabaha za mtunzi na jadi ya utunzi anayoiwakilisha. Huko Bukoba, kwa mfano, kivugo aghalabu hupaswa kuwa na mambo yafuatayo:

a) jina halisi na/au jina la sifa la mhusika; b) sifa za nasaba yake ya kuumeni; c) sifa za nasaba yake ya kuukeni; d) maelezo ya matendo matukufu aliyoyafanya; e) ahadi za kutenda makubwa zaidi kwa ajili ya mkubwa wake (mzazi, mtawala, umma, n.k.); f) tamati: 'kujikabidhi' rasmi kwa mkubwa.

Kwa asili vivugo haviandikwi, hutungwa papo kwa papo, lakini siku hizi baadhi ya watu wameanza kuvitunga (au kutungiwa) kwa kuandika, na halafu huvisoma au kusomewa wakati wa sherehe inayohusika (k.m. harusi). Haya ni maingizo ya kisasa ambayo bila shaka yanaashiria kubadilika, kama si kufa, kwa sanaa hii ya kale (Mulokozi 1989: 10-11).

Napenda kuongeza kwenye dondoo hili kwamba katika majigambo mbalimbali niliyowahi kuyasoma, nasaba ya kuukeni ndiyo inayozidi kusisitizwa, pamoja na

---

<sup>3</sup> Majigambo mengine hutokea katika ngojera na michezo ya kuigiza. Mengi sana hutokea katika tenzi, kama nilivyoonyesha katika mhadhara uliotolewa kwenye Mkutano wa 24 wa Isimu na Lugha za Kiafrika huko Chuo Kikuu cha Leiden (tarehe 29-31 Agosti 1994): *Self-praise in East-African Literature*.

kutumia majina halisi na amali za mji gambi. Aidha, siku hizi majigambo hufanywa mara nyingi sehemu za vijijini wakati wa sherehe za harusi au, hususan huko sehemu za Bukoba, hufanywa na wanafunzi wa shule za msingi wakati wa sherehe za kiserikali. Mengine hufanywa na waimbaji kama wapiga zeze, nanga, wacheza ngoma za kienyeji, au na watu binafsi bila ya kuzingatia sababu maalumu, k.m. wakati wa vinywaji, michezo, n.k. Majigambo ya aina hii hutokea mara nyingi mitaani. Kwa mfano mtu anaweza kujigamba kwa kujiweka katika ngazi fulani, akasema: Ile nyumba yangu niliyojenga mwaka jana nitaipangisha mzee mmoja aitwaye Juma. Katika usemi huu inawezekana huyo mtu hana hiyo nyumba, ila kutokana na mazungumzo ya watu waliokuwa wanaongelea nyumba, basi naye aliona aseme hivyo ili aonekane ana nyumba. Kujigamba kwa namna hiyo ndiko kunakoitwa *kujiketua*. Mtu mwingine anaweza kuvaa mavazi ya gharama, au kuwa na gari lenye thamani kubwa wakati hana uwezo wa kuwa na hivyo vitu. Basi anajilazimisha kuwa navyo na kujinyima vitu vingine kama chakula cha kutosha, n.k.<sup>4</sup>

Majigambo ya wakati wa sherehe ya harusi hufanyika baada ya bwana harusi kufunga ndoa na kujamiana na mkewe, ambapo huwa amethibitisha uume wake. Wakati wa sherehe hiyo msimamizi au shahidi wa bwana harusi au mtu yeyote yule aliyeteuliwa na kamati ya wazee kutoka upande wa bwana harusi ndiye anayeweza kujigamba kwa niaba ya bwana harusi. Wakati mwingine bwana harusi mwenyewe anaweza kujigamba kama ilivyokuwa zamani, ingawa inakuwa sio rahisi kwani shughuli yenyewe inahitaji mtu ambaye ni mkakamavu na msemaji sana, kitu ambacho kinaweza kumshushia hadhi bwana harusi. Katika sherehe hiyo mtu aliyepewa kazi ya kujigamba hupewa silaha na baba mzaa bwana harusi, ambayo hukabidhiwa kwa bwana harusi. Silaha hiyo inaweza kuwa mkuki, upinde na mshale, upanga, fimbo, kisu au bunduki. Inawakilisha ushujaa wa mtu aliyeoa. Maneno ya majigambo hutayarishwa mapema ili mtu anayejigamba aweze kuyapangilia vizuri. Wakati anapojigamba bwana harusi husimama akiwa ameshikilia silaha hiyo. Baada ya kujigamba, huwazungukia watu wote waliohudhuria sherehe hiyo na kuwashukuru. Maneno yaongelewayo huelezea hasa jina la bwana harusi, ndugu zake, uwezo wa familia, jinsi alivyompata bibi harusi, maisha yake toka azaliwe na jinsi gani atakavyoishi na mke wake. Huelezea ukweli wa jambo lililotokea huko nyuma au jambo ambalo sio kweli, ilimradi linamfanya huyo bwana harusi aonekane yuko katika ngazi ya juu, kwani anajiona kuwa ana uwezo mkubwa hasa baada ya kumpata bibi harusi. Ufuatao ni mfano mmoja uliotolewa na J. Rwatebula:

- (4) Mimi ni Juma Kamzora wa Mzee Shabani Kazimoto na Bi Ana Chakupewa. Nilizaliwa kijiji cha Ruhanga kisicho na milima. Nilizaliwa mwaka 1960 katika ghorofa ya tatu, nilianza kutembea nikiwa na umri wa mwezi mmoja. Mwaka 1961 nilianza shule ya Msingi na baadaye nikajiunga na Chuo Kikuu.

---

<sup>4</sup> Kufuatana na J. Rwatebula, majigambo haya hayatoi fundisho zuri sanasana, bali yanakuwa kama tishio tu, na yanapotosha.

Wakati wa likizo nilimkuta ndugu yangu anasumbuliwa na simba ambaye nilimwua peke yangu kwa kumnyonga.

Baada ya kumaliza masomo ya Chuo Kikuu niliamua kufanya kazi katika kampuni ambayo iliniteua kuwa meneja mkuu.

Siku moja nikiwa kazini nilikutana na binti Ashura nikamwambia kuwa nataka nimpose.

Kutokana nilivyokuwa nimevalia vizuri hakuweza kusita.

Leo hii nimefunga naye ndoa na amekuja kuishi katika familia ya mtu mwenye uwezo na shupavu.

Maana yake kwa ufupi ni kwamba mjigambi ametaja majina ya wazazi wake ambayo ni kweli. Lakini maneno mengine sio kweli: kutembea baada ya mwezi mmoja, kuanza shule baada ya mwaka mmoja, kuuu simba kwa kumnyonga, n.k.

Yapo majigambo mengi yanayoelezea jambo ambalo si la ukweli. Haya ni majigambo ambamo mtu hujiketua. Majigambo haya yana mafundisho ya aina fulani. Mfano halisi wa majigambo haya hupatikana vizuri katika mchezo mmojawapo uchezwao katika mkoa wa Kagera huko Tanzania uitwao *omutoro*. Nao vilevile huchezwa kama ngoma ya kienyeji ingawa mwanzo wake mtu mmoja hupiga ngoma kuonyesha kuwa kuna jambo lililotokea. Basi papo hapo mtu mmoja hutokea na kusema: "Nini imetokea?" Na mpiga ngoma humjibu na kusema: "Kumetokea jambo!" Baadaye tena mpiga ngoma hutamka jambo lililotokea. Basi huyo mtu huita wenzake na kusema: "Jamani njoni tumeingiliwa!" Basi wenzao waliojificha hutokea wakiwa wanaimba. Katika kikundi hicho hicho hutokea mtu mmoja ambaye huanza kujigamba.<sup>5</sup> Kwa hali halisi ilivyo majigambo haya hutoa fundisho la aina yake.

Majigambo ya wakati wa sherehe za kiserikali huhusika na jambo lililotokea. Mfano huu unachukulia hali halisi itokeayo huko vijijini hasa kwa wawindaji. Siku za sikukuu zikaribiapo, wawindaji hujitayarisha. Na siku moja kabla ya sikukuu huenda kuwinda. Ikiwa bahati nzuri wakauwa mnyama, basi mnyama huyo huletwa siku ya sikukuu na kucheze wakati wa majigambo. Mtu ahusikaye katika majigambo mara nyingi ni yule aliyemwua yule mnyama, au kiongozi wao, ingawa hiyo hutokea mara chache tu. Majigambo ya aina hiyo husimulia jinsi alivyo shupavu, hutoa hadithi nzima kuhusu jinsi mnyama huyo alivyouawa. Wakati huo huo huwa amezungukwa na wenzake wakiwa wanacheza ngoma. Baadaye huenda mbele ya mgeni rasmi kujigamba. Mwishowe mgeni huyo hutoa zawadi kwa kikundi hicho.

---

<sup>5</sup> Taz. vilevile Rubanza (1994: 3): "Vivyo hivyo uwanja wa matukio ya Majigambo huambatana na ngoma maalumu (*Amakondere/Omutoro*) ambayo ina mpigo wa kipekee, tofauti na mipigo mingine ya ngoma katika sherehe nyinginezo. Mipigo hii huwafanya waandamano na Mjigambi kuruka juu na kuinama chini kwa urari ulio sawia kiasi kilandanacho na mapigo ya ngoma. Baada ya hapo mmoja wao hujitokeza mbele ya Mtemi au mstahiki mwingine yeyote na kujigamba ama kwa kuzieleza sifa zake yaani zifa za Mjigambi mwenyewe au kueleza sifa za Mtemi au mkubwa huyo aliyekuwepo wakati huo".

Majigambo ya waimbaji ni kama yale ya wapiga zeze au nanga, wacheza ngoma za kienyeji, n.k. Nayo siku hizi hutokea katika wakati wa sherehe za kiserikali, ilimradi mara kwa mara sio lazima pawepo na sikukuu za kiserikali. Majigambo hayo hutokea wakati ule ule mtu anapokuwa anaimba au anacheza, na hutoa fundisho maalumu. Watu wengi huyasikiliza kwa makini kwa sababu hutolewa katika wimbo.

Katika sehemu zifuatazo tutahusika na muundo wa majigambo ya kishairi tu, yaani hayo ambamo mtungaji amejitahidi kuchagua na kupanga maneno yake kwa jinsi ya kupendeza, yaani ya kisanaa. Itaonekana kwamba kujigamba kishairi sio tu 'kujifanya unajua sana', kama inavyoelezwa katika kamusi, bali kitenzi hicho hukusanya maana za vitenzi vingine k.v. *kujitapa, kujiona, kujisikia, kujitukuza*. Pia hutumiwa kuelezea hali ya kujithamini, kujipa moyo, kustaajabia nguvu inayomwezesha mtu kutekeleza mambo makubwa, na ni njia mojawapo anayoitumia mjigambi kuwasifu na kuwashukuru watu anaowataja, kwa kuwa wao ndio waliomfanya afikie daraja la juu. Bila shaka mjigambi huthibitisha kuwa anajipenda na anafurahia nafsi yake, lakini pia hutoa ahadi kwa watu kwamba hizo sifa zake si za zamani tu, bali anazo kila muda. Ahadi hiyo humlazimisha kuonyesha uhodari na ushujaa katika maisha yake ya kila siku. Majigambo humsaidia mjigambi sana kisaikolojia na hata hao wanaosikiliza hupata nguvu.<sup>6</sup>

## 1. MUUNDO WA MAJIGAMBO

### 1.1 SEHEMU ZA JIGAMBO

Kwa kuwa majigambo ni fani ya fasihi simulizi, ambayo hutamkwa tu, tena kwa haraka sana, hakuna mgawanyiko kama ule unaopatikana katika mashairi andishi. Lakini tunapoyachambua kimaana na hata kimuundo, tunagundua mfumo maalumu, unaopatikana katika majigambo au sifo zote. Nao ni mgawanyiko katika sehemu ndogo ndogo zinazojirudia na ambazo ni fomula au semi fupi zenye maana nzima. Zipo fomula tofauti: baadhi ya fomula humkabili mjigambi (Mkabilisho), nyingine hutaja majina yake (Kirai nomino), nyingine hupanua maana ya majina hayo (Mtanuko), nyingine tena hutoa usimulizi kuhusu amali zake (Usimulizi), na nyingine huarifu kuwa jigambo limekwisha (Hitimisho). Ndani ya Usimulizi unaweza kupata mojawapo wa fomula zilizotajwa.

(5) O re: Ke sekitike se modumo      *Anasema: Mimi ni Mwenda-mbele-na-nyuma-atoaye-mlio-mkubwa*

---

<sup>6</sup> Kwa sababu hiyo, ingefaa sana hiyo ijulikane zaidi. Hapa Ubelgiji, watu wengi waliowahi kuhotubiwa juu ya majigambo ya Kiafrika huyafurahia sana. Kwa hiyo, tangu miaka miwili sasa, ninaalikwa mara nyingi katika shule na vikundi mbalimbali kuwafundisha watu jinsi ya kujigamba. Mwaka huu niliombwa na Wizara ya Elimu kuongoza semina kadhaa na kuwafundisha walimu wa adili wa shule za sekondari sana hiyo, ili nao waiingize katika masomo yao. Taz. Kabuta 1996, Kabuta and Milis 1996 na Legros 1996.

Ke kgomo yabo Mmaselatole  
E etše ge e re "phorohlo" e ragile  
kgamelo

*Mimi ni Mnyama wa Mmaselatole  
Hutenda kama vile ng'ombe  
aliyekasirika anayeipiga ndoo teke kwa  
mlio mkubwa*

(Pretorius 1989: 56)

Mpangilio uliotumiwa katika makala hii sio wa kawaida (ambao umeathiriwa na mpangilio wa ushairi andishi) bali unakusudia kutokeza sehemu za jigambo. Sio lazima fomula zote kuweko katika jigambo, lakini ni nadra Kirai nomino kutokuweko. Mfano wa 6 hudhihirisha jambo hili. Aidha, fomula fulani huweza kutokea katika sehemu mbalimbali za jigambo lile lile. Kwa mfano, fomula "Abayebembeile nkaita/Abasigaile enyuma echuchu yabaigala amaisho (*Waliotangulia niliwaua/Waliobaki nyuma vumbi iliwapofusha*)" hujirudia mara tatu katika jigambo liitwalo *Ukwebuga kwa Mugasha (kujigamba kwa Mugasha)* (Rubanza 1994: 57-63). Mara nyingi muundo fulani ndio unaojirudia, kama inavyodhihirika katika safu ya 3 ya mfano wa 6. Vilevile yadhihirika kwamba jigambo hugawanyika katika baadhi kubwa ambazo mpaka wake wa juu ni Mkabilisho (au Kirai nomino katika majigambo mengine). Kwa hiyo, zipo baadhi kubwa tatu katika mfano wa 6. Pia, fomula fulani au kibandili chake huweza kusafiri na kupatikana katika majigambo mbalimbali kwa njia ya kukopwa au kwa sababu wajigambi mbalimbali hushirikiana kinasaba.

6) Kihaya:

Naija  
Katuku Karubango  
Muini ntwekera embaizi

Naingia  
Katuku Karubango  
Mpini uwekwao shoka

nkagya omukibira kuiga entakwe  
Eibara banyeta Mutonyereza  
Kurwana

*Nilikwenda msituni  
Kuwindi wanyama  
Nikaitwa jina la Mtafuta-vita*

Mba  
njoka! nshamagi  
ngwa omumuti tingira byara  
na mpambo,

*Mimi ni  
Nyoka mwenye sumu kali  
Hurukia mtini lakini sina mikono  
na kucha*

Kampanantuka mpanantuka  
ndi muranzi.

*Nikiteremka chini huteremka  
nikiwa mtambaaaji*

Ninye  
kwezi kwayemire Karagwe  
Kyamutwara engoma ikaraa  
Mukama akugamba amyamire  
orwazi ayeshweka orutaro.

*Ni mimi  
Mwezi ulioandama Karagwe  
Kyamutwara la mgambo likalia  
Mtemi hunizungumzia wakati amelala  
kwenye mwamba akijifunika ungo*

Mpimbika! Kyamukazi, Bugabo  
nyita enju ya Kagoro Kairali  
Kenaindukire naita abe ebina  
abo omwa Rukora

*Huja kwa nguvu! Kwanyamukazi Bugabo  
niliua familia ya Kagoro na Kailali  
Nilipogeuka niliua familia  
Ya akina Rukora*

...

Abuka waitu mba nsingire Rugaba  
(Rubanza 1994: 39-40)

...

*Heshima ni yako Mtemi*<sup>7</sup>

Ili kuelewa muundo wa jigambo, inabidi tutumie istilahi isiyochanganya dhana au viwango vilivyo tofauti kabisa, hasa kiwango cha shairi na kiwango cha sehemu za shairi. Kwa mfano, mara nyingi watu hutumia neno lile lile, k.v. 'self-praise' (Kiingereza) au 'devise' (Kifaransa) kuliitia jigambo au sehemu ya jigambo. Nitatumia neno la *kijivugo* kuitia Kirai Nomino au Kirai nomino + Mtanuko, au Mkabilisho + Kirai nomino + Mtanuko, yaani sehemu ya shairi iliyo muhimu kabisa, ambayo hutumiwa kumsifia mjigambi. Lakini kumbuka, hiyo mofimu *-ji-* katika 'kijivugo' si kiwakilishi jirejee, bali huonyesha udogo (kama katika *kijisu*). Istilahi hii itatusaidia kutofautisha kabisa shairi na sehemu zake. Mifano mingine ni kama *Ndi...etajunjulwa*, *Ndi...efile*, *Ndi...atagangalwa*, hapo chini (7a). Kile tunachokiita shairi mara nyingi huwa ni mfululizo wa vijivugo tu ; mara nyingine huwa ni mkusanyiko wa vijivugo pamoja na sehemu nyingine zilizotajwa hapo awali. Kwa maneno mengine, kijivugo ni kifupi sana, wakati ambapo shairi ni mkusanyiko wa baadhi ya fomula (tuseme tatu nne). Pia, inabidi kutofautisha kijivugo na ubeti, ambao ni mkusanyiko wa maneno yaliyopangwa kufuatana na uchanganuzi fulani unaorudiarudia katika shairi (k.m. virari) na kwa kawaida huwakilishwa kimaandishi kwa mstari mmoja. Katika lugha nyingi sana za Kiafrika *vijivugo* huwa ni tanzu ya kifasihi inayojitegemea, ingawa mara nyingi neno lile lile hutumiwa kuitia fomula moja au mkusanyiko wa fomula, ambao ndio shairi.<sup>8</sup> Mtungo wa kijivugo kimoja au viwili tu si shairi, kwa sababu shairi huhitaji mfululizo wa mistari kadhaa, ambayo ndiyo msingi wa mizani.

Sasa tuchunguze baadhi ya nduni za kiisimu, kwa kutazama kiwango cha kifonolojia, kimofolojia, kileksika na kisintaksia. Kiwango cha wizani au pengine uchanganuzi wa ubeti, ambacho kinahitaji matini zilionukuliwa pamoja na toni na urefu wa sauti au sanasana sauti ya mshairi mwenyewe kwenye ukanda, hakitachambuliwa katika makala hii. Sehemu ya mwisho (2.5) itajadilia sintaksi ya kijivugo.

<sup>7</sup> Jigambo hili limedondolewa kutoka Rubanza 1994: 39-41. Katika tafsiri ya Kiswahili, niliandika maana ya jina Mutonyereza Kurwana, badala ya jina la Kihaya.

<sup>8</sup> Yafuatayo ni majina ya tanzu hiyo katika baadhi ya lugha: *makùmbù* (Ciluba), *lukùmbú* (Kilega); *magómbó* (Kikomo); *thandumunu* (Kiyaka); *pshiphato* (Kithonga); *zamu* au *jamu* (Kisonghay); *jammoore* (Kifula); *oriki* (Kiyoruba); *kirari* (Kihausa); *tige* (Kidogon); *yulaki* (Kiguro). Kwa Kiingereza neno litumiwalo sana ni *praise-name*, na kwa Kifaransa ni *devise*.



## 1.2 KIWANGO CHA KIFONOLOJIA

Mtungaji hutumia nduni zote za kifonologia za lugha, na bila shaka hutumia toni vilevile, ilimradi jambo hili halionekani mara nyingi kwa kuwa mashairi mengi hayakunukuliwa na hizo toni. Jambo linalojitokeza hasa ni marudiorudio ya baadhi ya silabi katika mstari, yaani takriri.

(7) a) Kihaya:

Ndi we'njoki Nyakajenje	<i>Mimi ni Nyuki Mwendapote</i>
Eyajunjuile etajunjulwa	<i>Ambaye huvuma hali awali hajavuma</i>
Ndi wa Kikenekelo na Nyungw'Ejwa	<i>Mimi ni wa Wanakopika-pombe na Kikombe-cha-matundu</i>
Kitachuga na Mbalo efile	<i>Ambaye hajamiani kwa mboo iliyokufa</i>
Ndi w'Omuganga atagangalwa	<i>Mimi ni Mganga ambaye hawangwi</i>

(Ndamugoba 1987: 25-26)

b) Kifula:

mbifee kam boosee kam	<i>Nipepeeni, nikandeni</i>
kokkee kam kore bodeeje!	<i>Nipeni vibuyu vilivyopakwa rangi nyekundu!</i>

(Seydou 1977: 226-227)

c) Kinyarwanda (takriri za toni na za mkaa wa sauti):

Ndi Rutaramana guhiga ndi Rutoneesha kuriinda, nd iintwáari y ímpezamihigo ntaraman ishem ábatágir ísheéja bátaraman amacúmu.

*Mimi ni Mshirika-kesha-kwa-ajili-ya-mabishano; mimi ni Mwanzishi-wa-ushindani; mimi ni Mmaliza-mabishano shujaa: hushiriki kwenye kesha kwa fahari, hali wasio na majivuno hushiriki kwa mikuki* (Coupez 1970: 100-101).

Toni zote katika sentensi ya kwanza ya mfano huu (*Ndi ... kuriinda*) ni toni chini: hii ni takriri ya toni. Aidha, majina *Rutaramana* na *Rutoneesha* yana idadi ile ile ya mora, yaani tano: hii ni takriri ya urefu wa sauti.

## 1.3 KIWANGO CHA KIMOFOLOJIA

Nduni muhimu ni marudiorudio ya nomino pekee, zikiwa halisi au za kubuni, ambazo hutumiwa kama majina ya mtungaji au ya watu alio na uhusiano nao. Nomino halisi mara nyingi hazitafsiriwi. Kwa kuwa aina zote mbili za nomino hizo zina uwezo wa kumsisimua msikilizaji au mghani mwenyewe, huitwa 'Majina ya kishairi'. Majina haya nimeamua kuyaandika kwa herufi kubwa mwanzoni kama

ilivyo kwa majina halisi mengine. Vitu au wanyama pia hupewa majina ya kishairi katika majigambo.

(8) Kihaya:

Buhembe bw'Ensa

*Pembe ya paa*

Mukuta irungu

*Atawalaye-mashambani*

Kujuju

*Mbung'o*

Kihangula bagumba

*Awazalishaye-wagumba*

Nkuba

*Radi*

Nkolola

*Kikohozi*

Kagogo

*Gamba*

(Ndamugoba 1987: 20)

Nyingi zaidi ni nomino ambatani, nomino ya kwanza ikiwa imenyambuliwa kutokana na kitenzi fulani, na ya pili aghalabu ni nomino ya kawaida. Mofimu zilizomo ni hizi: kiambishi awali cha nomino - shina - kiambishi tamati -a, ambazo zimeambatanishwa na nomino, au, kwa kifupi: *KN-S-a+N*. Kwa mfano, jina *Kihangula-bagumba* hapo juu huchambuliwa hivi: ki-hangul-a + bagumba. Kiambishi awali aghalabu huwakilisha ngeli za 7, 11, 12. Uhusiano baina ya neno la kwanza na la pili ni huo huo ulioko baina ya maneno yaliyo katika kishazi, k.m. *kuhangula bagumba*, yaani ni uhusiano baina ya kitenzi na yambwa. Mifano kadhaa ya nomino ambatani kama hizi hupatikana katika mashairi ya Kibantu, k.m. katika Ciluba, Kiyaka, Kiyaka, Kizulu, Kishona, Kinyarwanda, Kiswahili, n.k. Kwa mfano, katika Kiswahili, ngeli inayotumiwa sanasana ni hiyo ya 1:

(9) Muumba yote

Mwenda pote

Mshinda adui

Kama ilivyo kwa nomino ambatani nyingine, nomino hizi zina kivumishi husisho: (10) Simba Mla watu (yaani simba ambaye sifa yake ni kula watu).

Ngeli ya kivumishi husisho ni ile ile ya nomino itanguliayo, ingawa tungetarajia ngeli ya kwanza, kama ilivyo kawaida kwa majina ya watu. Upatanisho huu wa kishairi hupatikana pia katika lugha nyingi za Kibantu.<sup>9</sup>

(11) Ciluba:

Kalumba kàà Cikàngù

badala ya Kalumba wa Cikàngù *Kalumba wa Cikàngù* (Maalu-Bungi 1986: 108)

Cisùngù cyà Kapingaa Mvìdye

badala ya Cisùngù wa Kapingaa Mvìdye *Awashaye wa K. Mv.*

Lukòjì lwà manyaanù

badala ya Lukòji wa manyaanù *Lukoji Mchafu*

(Kabuta 1995: Ann.II, 55)

<sup>9</sup> Taz. Morris (1964: 23) kuhusu Kinyankore, na Koopman (1979: 76) kuhusu Kizulu.

(12) Kinyankore:

Ruhinda rwa Njunaki  
(Morris 1964: 23)

*Ruhinda (mwana) wa Njunaki*

(13) Kihaya:

Lukiza Iwa Kilomba

*Lukiza (mwana) wa Kilomba*  
(Ndamugoba 1987: 85)

Kishenya Malinzi kya Tibahwa

*Kishenya Malinzi wa Tibahwa (ibid. 22)*

Kashenge ka Rwabwita

*Kashenge wa Rwabwita (ibid. 20)*

Majina yote hayo hufanana kabisa na hayo yaitwayo lakabu. "Lakabu ni majina ya kupanga ambayo baadhi ya watu hupewa au hujipatia kutokana na sifa zao za kimwili, kinasaba, kitabia au kimatendo. Majina haya huwa ni maneno au mafungu ya maneno yenye maana iliyofumbwa. Mara nyingi majina haya huwa ni sitiari, ambayo humsifia mhusika:

(14)

Mukwavinyika (Kihehe)

*Mtekaji wa Nyika (Mkwawa)*

Ka-Itaba-Mbibi (Kihaya)

*Mtoto-wa-mchanganya-mipaka*

Mkuki Uwakao (Jomo Kenyatta)

Simba wa Yuda (Haile Selassie)

Nyungu ya Mawe (Mtemi wa Ukimbu, Unyamwezi)

Mti-Mkavu (Jenerali Mayunga).

Karibu washairi wote mashuhuri wa Kiswahili, wa kale na wa sasa kama R. Shaaban, M. Hanasa, M. Mnyampala, S.A. Kandoro, A.S. Zakwany, K.A. Khamis, E. Kezilahabi, M. Mulokozi, n.k., wameyatimia majina haya ya kishairi" (Mwansoko 1981: 46-57).

Vijana wa Kizulu huyatumia sana majina kama haya, ambayo huitwa *izibongo*, katika michezo ya mpira, ya ndondi, ngoma, katika mapigano au katika juhudi zao za kujipendekeza kwa wasichana:

(15)

a) uZindlelazimazombe

*Njia ya Kupindukapinduka*

b) uMehlabovu okubheka maqede  
ushaywe uvalo

*Macho Mekundu, ambayo  
uyatazampo, unashikwa na hofu*

c) uMuntomude akaliboni izulu

*Mtu Mrefu, ambaye haoni mbingu*

d) uKhozi olumaphiko olucosha

*Hajivale Mwenye Mabawa,*

ichwane ngokuphazima kwezo

*anyakuaye kifaraga kwa ghafla*

e) 'Young Destroyer'

*Kijana Mharibifu*

(Koopman 1988: 43-48)

Jambo la mwisho kuhusu mofolojia ni kuwa vitenzi huchukua vipatanishi vya nafsi ya kwanza, umoja au wingi.

## 1.4 KIWANGAO CHA LEKSIKA

Nduni kubwa kileksika katika aina hii ya ushairi ni utumiaji wa sitiari. Sitiari nyingi ni hizo zinazonyesha nguvu, ukali, ukatili, ugumu, kama vile moto, radi, nyuki, baridi, chui, n.k. Mara nyingi hufuatwa na kipambanuzi kinachotoa maelezo zaidi juu ya sitiari hiyo:

(16)

Ndi Nkuba Kachwachwaita	<i>(Mimi) ni Radi Akimbiaye kasi</i>
Ndi Nkolola Mpondeleza abana	<i>(Mimi) ni Kikohozi Awafuataye watoto</i>
Nzilana n'Omukazi azaile	<i>Simgusi mwanamke aliyezaa</i>
Ndi kagogo	<i>(Mimi) ni Gamba la mti</i>

(Ndamugoba 1987: 25)

(17) Ifuatayo ni mifano mingine kutoka majigambo mbalimbali ya Kihaya:

- a) Nyuki wa Nyakajenje
- b) Ugali wenye ladha mbaya
- c) Pembe ya paa
- d) Mbung'o (ninampanda mbogo mgongoni)
- e) Baridi (Nalala nyumbani mwa matajiri/Hata kama wamezifunga kwa vioo/Na pazia/Nitaingia)
- f) Chui wa madoadoa
- g) Ngozi ya nyoka itishayo
- h) Kuni iliyokauka
- i) Swila wa Kiyondo aonaye gizani

(18) Kimongo:

- |                                     |  |
|-------------------------------------|--|
| a) Emí bokombe w'ônkúndu            | <i>Mimi Mlangamia Mshindi (Ekombe 1991: 452)</i>     |
| b) Emí mpóngó __,ea lokóla lotálé o | <i>Mimi Kozi Mwenye-kucha-ndefu (Mamet 1962: 47)</i> |

(19) Kiluba:

Ami Sunkutu kabanda,	<i>Mimi Simba-wa-msituni</i>
Kalobwe muntabangula bwanga	<i>Asiyeogopa kurogwa</i>
Ye ukubangula mutwe wa bukala	<i>Anayetangulia kula mboo ya mateka zake</i>

(Chiwale 1962: 27)

(20) Nduni kubwa nyingine ni utumiaji wa chuku, yaani kujizidishia sifa au kutia chumvi:

- a) Ndimi mwana wa Kiitana wa Mibalula Aliyegombana bila ya kuwepo
- b) Ndimi Kakonka apasuaye mioyo

- c) Niliirukia maiti huku nikiwabeba wagonjwa
- d) Bibi mzee na mkwe wake wa kike Nikazungumza nao moja kwa moja wakakubali Nikajamiana nao
- e) Nikajamiana na mtoto mchanga na kumpa mimba Nikaitwa Awazalishaye-wagumba
- f) Ndimi Mfalme wa wanyama wote

Nduni hii ya kujizidishia sifa hupatikana pia katika mashairi maalum ya Wanyankore na Wanyarwanda, ambao ni majirani wa Wahaya, vilevile katika Kiigbo (Nigeria), Kishona (Zambia) na katika lugha nyingine za kusini mwa Afrika.

(21) Kishona:

Ndíní Hódzamutsipa,  
Mutakuramombe, mbúdzíhata.

*Mimi ni Mvunja-shingo  
Abebaye-ng'ombe akitumia mbuzi  
kama kata*

Ndinókuróvá, ukapazika mhúmbá  
yemwóyo.

*Nitakupiga na sanduku la roho yako  
litapasuka*

(Hodza & Fortune 1979: 366)

(22) Kinyankore:

Ruhimbwá ndemera nti ómu ihangá

*Asifiwaye niligombana kwa  
ushujaa vitani pamoja*

na Rutaahira

*na Mwangushaji*

Ruhambisa-ábiri nkatoorwa ómutánda

*Anayechukua-kwa-nguvu-akiwa-  
na-mikuki-kwenye-mikono-yote-  
miwili nilijitokeza niking'aa katika  
vazi langu la pamba*

(Morris 1964: 43)

(23) Kiigbo:

Abu m:

*Mimi ni:*

Enu di ulu

*Mahali-pa-juu azaaye matunda*

Agbu na-eme eze

*Kamba ya kupandia ifikishayo kwenye kilele  
cha mnazi (yaani cheo cha 'eze')*

Mma na-egbu ego

*Kisu kivunacho pesa*

Uba shi n'enu.

*Utajiri kutoka juu*

(Egudu & Nwoga 1973: 32)

## 2. SINTAKSI YA KIJIVUGO

Kijivugo ndiyo sehemu muhimu kabisa katika majigambo. Hutokea katika majigambo karibu yote Afrika, na kama tulivyokwisha sema hapo awali, majigambo mengi huwa ni mfululizo wa vijivugo tu. Kwa hiyo lazima tuchambue sintaksi yake kwa undani. Kwa kuwa jina (la kishairi) ndicho kirai muhimu kabisa katika kijivugo, viambajengo vingine hufasiliwa kufuatana na kirai hicho. Nyanja kubwa nne zabainishwa katika kijivugo: Mkabilisho, Jina, Kipambanuzi na Mtanuko. Jina mara nyingi ni neno nyambuliwa (k.m. Msuluhishi, Msemaji); neno ambatano, neno la kwanza likiwa ni neno nyambuliwa (k.m. Mfanya urafiki, Mtafuta vita, Mpigania haki); neno la kisitari (k.m. Nyoka, Jani); au neno halisi lo lote. Uwanja wa jina na wa kipambanuzi huweza kutokea mara mbili au tatu katika kijivugo kile kile. Mkabilisho ni neno lo lote k.v. *mimi (ni)*, *ndimi*, *naingia* n.k., linalotangulia jina. Kipambanuzi ni neno au fungu la maneno linaloonyesha sifa ya kipekee ya jina. Mara nyingi huwa ni kivumishi, jina nyambuliwa, kirai na kiunganishi tegemezi au kishazi rejeshi. Mtanuko ni sentensi yo yote ile ipanuayo zaidi maana ya jina kwa kutoa maelezo juu ya mhusika. Mara nyingine, kama katika vijivugo vingi vya huko Afrika Magharibi, mtanuko hujitegemea, bila kuwoko kwa jina lo lote. Kwa hiyo, vijivugo vyote vilivyoundwa kwa msaada wa jina huitwa 'vijivugo vya kijina', na hivyo ambavyo vimeundwa kwa kitenzi tu, 'vijivugo vya kitenzi'. Jedwali 1 hapo chini ni muhtasari wa sintaksi ya vijivugo. Katika mifano iliyotolewa, herufi kubwa (A, B, n.k.) huonyesha aina ya kijivugo, na nambari isiyo katika mibano duara huonyesha uwanja. Mifano:

**Jedwali 1.** Sintaksi ya kijivugo.

AINA	1 Mkabilisho	2 Jina	3 Kipambanuzi	4 Mtanuko
A	±	+	+	+
B	±	+	+	-
C	±	+	-	+
D	±	+	-	-
E	±	-	+	-
F	±	-	-	+

### 2.1 (MKABILISHO) + JINA + KIPAMBANUZI + MTANUKO:

(24) Kihaya

2 Omuganga

3 atagangalwa

4 Mulengelezi nkalengela

*Mganga*

*asiyegangwa*

*Mwenye-macho-makali, naweza*

*kumwona*

(Ndamugoba 1987: 26)

(25) Kishona:

- 1 Ndíní
- 2 Hódzamutsipa
- 3 Mutakuramombe, mbúdzíhata.
  
- 4 Ndinókuróvá, ukapazika mhúmbá yemwóyo

(Hodza & Fortune 1979: 366)

*Mimi ni*  
*Mvunja-shingo*  
*Abebaye-ng'ombe akitumia mbuzi*  
*kama kata*  
*Nitakupiga na sanduku la roho*  
*yako litapasuka*

(26) Ciluba:

- 2 Diitu
- 3 Kàsòòlasoolà
- 4 Wa kusòòla dyàmwosha mpesà

(Kabuta 1995: Ann.II, 25)

*Msitu*  
*Usiofyekwa*  
*Aufyekaye huumwa na upupu*

## 2.2 (MKABILISHO) + JINA + KIPAMBANUZI:

(27) Kihaya:

- a) 1 Ndi
- 2 Nkuba
- 3 Kachwachwaita

(Ndamugoba 1987: 25)

*(Mimi) ni*  
*Radi*  
*Akimbiaye kasi*

- b) 1 Ndi
- 2 Igambuluzá
- 3 nkagambuluzá Omuganda

(Ishemoi 1978: 30)

*(Mimi) ni*  
*Mpiganaji shujaa*  
*aliyempiga Mganda*

(28) Kiyaka:

- 2 M'tá
- 3 káteela kháánda
- 2 M'dimí
- 3 kádimina nzála

(Ifwanga-Wa-Pindi 1975: 129)

*Mgombanaji*  
*awagombaniaye nduguze*  
*Mkulima*  
*alimiaye njaa (ili kuikomesha)*

(29) Kiluba:

- 2 Nkonda bilo
- 3 Wakondele ubuleyi ne butombo
- 2 Mutunda
- 2 Mwabilwa Ntanda
- 3 Bashele baabilwa mbushi

(Chiwale 1962: 16)

*Mnyang'anyi*  
*Anyang'anyaye nchi kwa nguvu*  
*Kichuguu*  
*Mpewa-nchi*  
*Ilhali wengine hupewa mbuzi*

- (30) Ciluba:  
2 Kapyà *Mwanga*  
3 kàà cimunyi *wa mienge*  
3 Kààkamunynà bakàjì mu njila *Uliyowamulikia wanawake njiani*

- (31) Kiswahili  
1 Ni  
2 Mwana asadi  
3 Mtanganya moyo wa kufa  
(Harries 1962: 190)

### 2.3 (MKABILISHO) + JINA + MTANUKO:

- (32) Kihaya:  
1 Ndi  
2 Matoju *Mimi ni (jani la) Matoju*  
4 Ndibatwa bwankya *Hukanyagwa asubuhi*  
4' bwamushana nkalana *Mchana huwa tena makali*  
(Ishemoi 1978: 38)

- (33) Kinyankore:  
2 Ruhimbwá *Asifiwaye*  
4 ndemera nti ómu ihangá na Rutaahira *niligombana kwa ushujaa vitani pamoja na Mshindi*  
(Morris 1964: 43)

### 2.4 (MKABILISHO) + JINA:

- (34) Kizulu:  
uZindlelazimazombe *Njia ya Kupindukapinduka*  
(Koopman 1988: 44)

### 2.5 MKABILISHO + KIPAMBANUZI

Muundo huu hupatikana sana katika mashairi simulizi ya lugha nyingi za Kibantu. Mara nyingi sana shina lililo katika Jina hutokea vilevile katika Kijalizo ambacho ni kishazi rejeshi:



(35) Kihaya:

- a) 1 Ndi  
2 wa Lukiza  
2' Lukiza lwa Kilomba  
Kishenya Malinzi kya Tibahwa  
Kashenge ka Rwabwita  
(Ndamugoba 1987: 25)

*Mimi ni (mwana) wa Lukiza  
Lukiza (mwana) wa Kilomba  
Kishenya Malinzi wa Tibahwa  
Kashenge wa Rwabwita*

- b) 1 Ndi  
2 Kashenge  
3 ka Rwabwita  
1 Ninye  
2 Buhembe  
3 bw'Ensa

*Mimi ni  
Kashenge  
wa Rwabwita  
Ndimi  
Pembe  
ya paa*

- c) 1 Mba  
2 Kakonda  
3 Nyat'Omutima  
(ibid. 20)

*Ndimi  
Kakonka  
Apasuaye-mioyo*

- d) 2 Nkuba  
3 kachwachwaita  
2 Nkolola  
3 mpondeleza abana  
(ibid. 25)

*Radi  
akimbiaye-kasi  
Kikohozi  
kifuatacho watoto*

## 2.6 MTANUKO:

(36) Kifula:

- 4 mbifee kam boosee kam  
4' kokkee kam kore bodeeje!

*Nipepeeni, nikandeni  
Nipeni vibuyu vilivyopakwa rangi  
nyekundu!*

(Seydou 1977: 226-227)

\* Sehemu ya makala hii ilitolewa kama mhadhara kwenye Semina ya Nane ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Bayreuth, tarehe 26-27 Mei 1995. Shukrani ziwaendee watoa taarifa wangu J. Rwatebula (Chuo Kikuu cha Brussels) na J. Rwabyo (Dar es Salaam), M. Mulokozi (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam) kwa msaada wake nilipokuwa nikifanya uchunguzi huko Dar es Salaam, na M. Konter (Chuo Kikuu cha Leiden) kwa kusoma mswada.

## NYONGEZA

## I. MIFANO MINGINE

Katika mifano ifuatayo, virai nomino ambavyo ni majina ya kishairi vimeandikwa kwa herufi kubwa. Vifupisho vifuatavyo vimetumiwa kuwakilishia fomula: Kij = kijalizo; KN = kirai nomino; Mkab = mkabilisho; Mtan = mtanuko; Usim = usimulizi.

## 1. Kisuthu-Kaskazini:

1. Ke nna Mašišimale a gabo Mošiane tlou a Mabasa,	<i>I am the Adamant person of the place of Mošiane, Elephant of Mabasa</i>	Mkab+ KN+Kij+ KN
2. Tlou ya manaka ke eme Marutle gabo Lekgolane,	<i>Elephant-bull, I stand at Maruthe, place of Lekgolane,</i>	KN+Usim
3. Ke šišimetše ke etša leltlapa lefsika lapeng labo Matobole.	<i>I stand firm as a rock, in the family of Matobole.</i>	Usim
4. Gale borangwen le fetōša batho batseta,	<i>By the way, you, my uncles, turn people into peasants,</i>	Usim
5. Ge le tšea boSebape morwa Mmakhudu la etiš a pele.	<i>When you moved people like Sebape, the son of Mmakhudu, to the front</i>	Usim
6. Ke sekitike se modumo,	<i>I am the One-who-moves-to-and-fro-with-a-mighty-sound,</i>	Mkab+KN
7. Ke ketiša mampiriri ye mentši,	<i>I move around, thick-haired,</i>	Usim
8. E ba ergo meriri ya ka e tšame e boolwa Matebeleng.	<i>My hair, which they say gets shaved even by the Ndebeles.</i>	Usim
9. Mapogo le Kwalepe 'a Mapulana ba mpootše,	<i>Mapogo and Kwelepe of Mapulana shaved me,</i>	Usim
10. Ba ntšhia meriri dikgofe.	<i>And left some tufts behind.</i>	Usim
11. Ba re: Kgarebe tša Makotopo di a lla.	<i>They say the young Makotopo women are complaining.</i>	Usim
12. Di re: Bauba ga se wa go hlwa le motho.	<i>They say Bauba is not one to spend the day with.</i>	Usim
13. O r'eng a enwa 'hlama	<i>Why does he drink our beer in</i>	Usim

tša rena a homotše?	<i>silence?</i>	
14. Bauba mmoetšeng Lokase, ga gabo-mogolo Mtsha,	<i>Take Bauba back to Lokase, the place of his maternal grandparents, Matsha,</i>	Usim
15. O re: Ke ya le mme Matsha,	<i>He says: I am going to Matsha with Mother,</i>	Usim
16. Gabo šatalla 'a šata, šetla la nku le a betlwa,	<i>Where a sound of sounds is heard, the soft bone of a sheep is cut out,</i>	Mtan
17. Moko re gafela bašemane ba dipudi.	<i>That marrow in the bones we give to the goatherds.</i>	Usim
18. O re: Ke sekitike se modumo,	<i>He says I am the One-who-moves- to-and-fro-with-a-mighty-sound,</i>	Usim
19. Ke kgomo yabo Mmaselatole,	<i>I am the Beast of Mmaselatole,</i>	Mkab+KN
20. E etše ge e re 'phorohlo' e ragile kgamelo,	<i>He acts like an angry cow which kicks the bucket with a pang-pang sound</i>	Usim
21. Leleke la ga Mphahlele le weditše ka meetseng.	<i>The tin of Mphahlele's place it lets fall into the water.</i>	Mtan
22. Ke mo go tlogo lethebeswane la noka a Tubatse,	<i>That's me: the Wave of the river of Tubatse,</i>	Mkab+ KN+Kij
23. O re: Ga ke theboše, ke theoša le molapo	<i>He says: I do not go under, I lead down the river.</i>	Usim Mkab+KN +Kij+KN
24. Ke Maramnyane a mmoto 'a Tšate, theledi a Marota,	<i>I am the Lizard of the hill of Tšate, the Slippery-one of Marota,</i>	Usim
25. E a rego ke ba theletše ba šala ba swara ba šele	<i>The one who says I evaded them while they continued to capture the wrong ones,</i>	Usim
26. Ba šala ba swara Bapedi ba-epa-tšhoga ka legong. (Pretorius 1989: 56-57)	<i>They remained, catching the Pedis, the bulb-diggers, with firewood.</i>	
2. Kisuthu-Kaskazini:		
1. Ke Maputle ka mpapedi a selepe,	<i>I am the Traveller with two-bladed axe,</i>	Mkab+ KN+Kij
2. Fase ga sehlakahlaka ke ile ka hlakahlaka,	<i>Under the Island I once suffered,</i>	Usim
3. Fase ga mogokare ka gokara selepe,	<i>Under the Cape willow I carried an axe,</i>	Usim

4. Fase ga modibo ka dibola naswa,	<i>Under the tree (Modibo) I turned the black cow over,</i>	Usim
5. Ge nkabe kgoši a nthata,	<i>If the king should love me,</i>	Usim
6. Nkabe a nkabela mathari,	<i>He would give me women,</i>	
7. Ka fela ke ya kua le kua,	<i>Then I would go hither an thither,</i>	Usim
8. Ba re: Moloto ka mpapedi morwa kgoši.	<i>They would say: Moloto, the double- stomached, son of a king.</i>	Usim

(Pretorius 1989: 65)

### 3. Kiswahili:

Mbonapo harubu chiugua nawa na afa Kawa na furaha ja harusu ya mzafafa Kaekeza moyo kwa Muungu nisikhilafa		Usim
Ni/Mwana asadi mtanganya moyo wa kufa kwa kucha khazaya na adui kumbona nyuma		Mkab+KN+Mtan
Napa kwa Muungu na Muungu ndiye kiapo Nampenda mtu pindi naye anipendapo Bali nguu yangu pindi ari ambwagazapo		Usim
Ninga/Mwana kozi/sioneki niwakuapo/ni/Muwi wa nyuni/nawa- kua katika yama.		Mkab+KN+Mtan+ Usim+KN+Usim
Wallahi nithika sya yangu si maongope Teteapo cheo kiwa mwiu nawa mweupe Nimpapo uso aduiya shati akupe		Usim
Ninga/Mwana tai/shirikene na mwana tope na mlisha yani zenye tani na singulima. (Harries 1962: 190-193).		Mkab+KN+Mtan

### 4. Kiswahili:

Mimi ni/Kimbunga king'oacho miti mikubwa na midogo		Mkab+KN Mtan
Si/Upepo wa kawaida ufanyao miti ijipinde na kurudia hali yake mara upepo unapopita		Mkab+KN Mtan
Mimi sio/Upepo ulioletwa na wapita njia ambao mara uligeuka sumu ukaupondaponda mwili wangu (Lihamba et al. 1982: 10)		Mkab+KN+Mtan

5. Kiswahili:

Naingia Mwamba wa miamba  
Jiwe gumu lipasualo mengine  
Nilizaliwa shujaa, mkono mmoja  
nimeshika silaha za vita  
na mkono wa pili dawa za uganga.

Mkab+KN  
KN+Mtan  
Usim

Ninawatia usingizi  
Wakati mimi nazidi kupaa angani.  
Mimi ni Ncha ya mkuki  
sipigwi konzi.  
Natumia silaha na dawa  
za uganga kuwanyamazisha  
(Lihamba et al. 1982: 12)

Usim  
Mkab+KN  
Usim  
Usim

6. Kiswahili:

Jina langu nakwambia  
ndi mimi Shekhe Alia  
ibunu amu Nabia  
Muhamadi 'IBashiri.

Mkab  
Mkab+KN  
Mtan

Ndimi Simba wa Mungu  
ndimi Mkusa matungu  
ndimi Muwanya mafungu  
ndi Mpangua ari.

Mkab+KN  
Mkab+KN  
Mkab+KN  
Mkab+KN

Ndimi Aba 'IHasani  
ningiapo utamboni  
huwadhili fursani  
wasijua tadibiri.  
(Mgeni : 1980: 80)

Mkab+KN  
Usim

7. Kinyankore:

1. Ruhimbwá ndemera nti ómu ihangá na Rutaahira	KN+Usim
2. Ruhambisa-ábiri nkatoorwa ómutánda	KN+Usim
3. Rukaré guunyahá haraingwa na Rwihira-ngabo	KN+Usim
4. Ruzingizá naitangirá Bihanga na Bitembe	KN+Usim
5. Kaanyabareega nkeekwata na Bukwakwa	Usim
6. Bantura yaakwata ékyéshongoro ngu tubingye.	Usim
7. Oruhindá nkagikubuuza nti órubángo na Rwamujonjo	Usim
8. Ábanyóro baatiina ómukaituranó gwa Kahenda	Usim
9. Énkókó za Karembe zantanga kujúga	Usim
10. Rukiná mbakumbizá Nyamizi na Rutasikwa.	Usim
11. Nkangá nkarikwatá aha muhúnda	Usim
12. Kanyegyero bayecura Ruboherá	Usim
13. Nikwó naabaire ntarugá mu naama y'Ábahinda na Rwangomani	Usim
14. Rushahúza nkabá mmuhambire ngu tutwarane.	KN+Usim

1. *I Who Am Praised thus held out in battle among foreigners along with The Overthrower;*
  2. *I Who Ravish Spear In Each Hand stood out resplendent in my cotton cloth;*
  3. *I Who Am Quick was drawn from afar by lust of the fight and with me was Repulser of Warriors;*
  4. *I Who Encircle The Foe, with Bitembe, brought back the beasts from Bihanga;*
  5. *With Bwakwakwa, I fought at Kaanyabereega,*
  6. *Where Bantura started a song that we might overcome them.*
  7. *Thus with my spear, I and Rwamujonjo conquered Oruhinda;*
  8. *The Banyoro were afraid on the battlefield of Kahenda;*
  9. *The cocks of Karembe had already crowed;*
  10. *I Who Am Nimble with The One Whom None Can Dislodge felled them at Nyamizi.*
  11. *At Nkanga, I seized my spear by its shaft-end;*
  12. *At Kanyegyero, I The Binder Of Enemies took them by surprise;*
  13. *Thereafter was I never excluded from the counsels of princes, nor was Rwangomani;*
  14. *I Who Rescue With The Spear had seized him so that we might fight together.*
- (Morris 1964: 42-45)

## II. ISTILAHU

Zifuatazo ni tafsiri kwa Kiingereza za maneno machache ya kitaaluma yaliyotumiwa katika makala hii na ambayo labda yangeweza kutatanisha kidogo kwa kuwa hayasikiki sana. Maneno machache yaliyopendekezwa kwa ajili ya makala hii yametanguliwa na kinyota. Dhana nyingine mpya zimefasiliwa mahali zilipotajwa katika makala.

isimu ushairi	<i>poetics</i>	marudio	<i>repetition</i>
istiari	<i>metaphor</i>	*maudhui	<i>theme; content</i>
jirejee	<i>reflexive</i>	msitari	<i>line</i>
kiambishi tamati	<i>suffix</i>	muundo	<i>structure</i>
kiambishiawali	<i>prefix</i>	nduni	<i>characteristics</i>
*kijivugo	<i>praise-phrase</i>	ngeli	<i>class</i>
*kirudio	<i>motif</i>	nomino ambatani	<i>compound noun</i>
kina	<i>rhyme</i>	rara	<i>ballad</i>
kishazi	<i>phrase</i>	taaluma ya ushairi	<i>poetics</i>
kitenzi	<i>verb</i>	takriri	<i>assonance</i>
kiunganishi-	<i>connective-</i>	sifo	<i>panegyrics</i>
tegemezi	<i>pronoun</i>	tamathali za usemi	<i>figures of speech</i>
kivugo	<i>self-praise</i>	tanzu	<i>genre</i>
kivumishi	<i>adjective</i>	uchanganuzi	<i>scansion</i>
kiwakilishi	<i>pronoun</i>	utendi	<i>epic</i>
*mada	<i>topic</i>	wizani	<i>rhythm</i>
majigambo	<i>self-praise</i>	shamirisho	<i>object</i>
mapigo	<i>metre</i>		

MAREJEO<sup>10</sup>

Balisidya, M.L. 1987.

*Tanzu na Fani za Fasihi Simulizi. Mulika* Na. 19: 2-10. TUKI, CKD, Dar es Salaam.

Chiwale, J.C. 1962.

*Central Bantu historical texts III: Royal Praises and Praise Names of the Lunda Kazembe of Northern Rhodesia; The Meaning and Historical Background.* Rhodes Livingstone Institute, Lusaka.

Coupez, 1970.

*Littérature de cour au Rwanda.* OUP, Oxford.

Egudu, R.N. and Nwoga, D.I. 1973.

*Poetic Heritage: Igbo Traditional Verse.* Nwankwo-Ifejika and Co. Ltd, Enugu.

Ekombe, 1991.

*Les anthroponymes mongo dans l'ÚpopÚe Nsong a Lianja. Annales Aequatoria* 12, pp. 447-455. Bandundu.

Harries, L. 1962.

*Swahili Poetry.* OUP, Oxford.

Hodza, A.C. and Fortune, G. 1979.

*Shona praise-poetry.* The African Library of African Literature, Oxford.

Ifwanga-Wa-Pindi. 1975.

*Les genres liés de la littérature orale yaka: Essai d'étude stylistique.* unpubl. M.A. dissertation, Université Nationale du Zaïre, Lubumbushi.

Ishemoi, J. 1978.

*The Heroic Recitations of the Bahaya of Bukoba.* Unpubl. M.A. dissertation, UD, Dar es Salaam.

Kabuta, N.S. 1995.

*La formule et l'autopanegyrique dans les traditions orales africaines. Etude structurelle.* Tasnifu ya Ph.D., Université Libre de Bruxelles.

1996 *L'autolouange dans les traditions orales africaines, Entre-vues, Revue trimestrielle pour une pédagogie de la morale*, Na. 31-32: 97-110, Bruxelles (muhtasari wa makala hii umetolewa tena katika jarida **Initiations**, Na. 13, Bruxelles, novemba 1996).

1997 *Le désir de gloire, Africana Gandensia*, Gent (forthc.).

Kabuta, N.S. and Milis, M. 1996.

*Autopanegyrique, Entre-vues, Revue trimestrielle pour une pédagogie de la morale*, Na. 31-32: 91-92, Bruxelles.

*Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* 1981.

TUKI, CKD, Dar es Salaam.

---

<sup>10</sup> CKD: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; OUP: Oxford University Press; TPH: Tanzania Publishing House; TUKI: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili; UD: University of Dar es Salaam.



*Kiswahili Sekondari*. 1988.

Tanzu za Fasihi, Taasisi ya Ukuzaji Mitaala, pp. 119-166, Dar es Salaam.

Legros, K. 1996.

*Leçon: Rédiger son autopanegyrique. Entre-vues, Revue trimestrielle pour une pédagogie de la morale*, Na. 31-32: 93-96, Bruxelles.

Lichtheim, M. 1975.

*Ancient Egyptian Literature, Vol. I: The Old and Middle Kingdoms*. University of California Press, Los Angeles.

Maalu-Bungi, 1986.

*MePn'Ó bukolP : Poésie d'exaltation lubÓ*. Buzat Editions, Lubumbashi

Koopman, A. 1979.

*The Linguistic Difference Between Nouns and Names in Zulu. African Studies*, pp. 67-80. WUP, 38/1., Johannesburg.

1988 *The Praises of Young Zulu Men. Theoria*: 60-74.

Lihamba, A., Balisidya, N., Mhando, P. 1982.

*Harakati za Ukombozi*. TPH, Dar es Salaam.

Mamet, 1962.

*La l'Úgende d'Iyanja: Texte ntomba*. Office International de Librairie, Bruxelles.

Mgeni Bin Faqihi. 1980.

*Utenzi wa Rasi 'Lghuli*. TPH, Dar es Salaam.

Morris, 1964.

*The Heroic recitation of the Bahima*. The Clarendon Press, Oxford.

Mulokozi, M.M. 1989.

*Tanzu za fasihi simulizi. Mulika*, Na. 21: 1-24. TUKI, CKD, Dar es Salaam.

Mwansoko, H.J.M. 1981.

*Lakabu (Majina ya Kishairi), Lugha Yetu, Tuisome Tuijue. Bakita*, Na. 38: 46-57. Dar es Salaam.

Ndamugoba, S.R. 1987.

*The Significance of the Praise Poetry among the Bahaya, a case study of Kyamutwara, Kagera Region*. Unp. M.A. dissertation, UD, Dar es Salaam.

Pretorius, W.J. 1989.

*Aspects of Northern Sotho Poetry*. Via Afrika Limited, Pretoria.

Rubanza, Y.I. 1994.

*Fasihi Simulizi: Majigamba (Ebyebugo)*. Dar es Salaam University Press, Dar es Salaam.

Seydou, Ch. 1977.

*La devise dans la culture peule: évocation et invocation de la personne*, Cf. G. Calame-Griaule, Mhariri, **Langage et culture africaine, essai d'ethnolinguistique**. F. Maspéro, Paris.